BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 10 Juni, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

107. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Jeshi la Polisi Mkoa Mjini Magharibi limepata mafanikio mangapi kwa kesi zilizopelekwa Mahakamani kwa kipindi cha miaka miwili nyuma.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

214. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kiasi gani sheria mbali mbali zinazopitishwa katika Baraza la Wawakilishi zinazingatia kipengele muhimu cha Haki za Binadamu.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

42. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana wa Zanzibar wanaomaliza masomo katika elimu ya juu katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi. Changamoto kubwa ni kwamba vijana wengi ambao wamemaliza masomo bado hawajaweza kupata ajira rasmi jambo linaloleta maswali mengi kwenye mifumo yetu ya elimu.

(a) Je, ni ipi takwimu rasmi ya vijana waliohitimu vyuo mbalimbali ambao hawajaweza kujiajiri au kuajiriwa.

(b) Je, ni taaluma zipi zina fursa nyingi na zipi zina fursa chache za kujiajiri au kuajiriwa baada ya kuhitimu.

(c) Je, kwa kipindi cha miaka minne iliyopita ni ajira ngapi zilipatikana katika sekta rasmi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

99. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tathmini ya ongezeko la makusanyo ya kodi iko vipi kwa sasa.

256. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika taasisi za Serikali kumekuwa na hoja mbalimbali za kikaguzi zinazohusu kufanyika kwa malipo yasiyokuwa na vielelezo.

Je, ni kwa kiasi gani matumizi ya mifumo yamekuwa suluhisho la kupunguza ama kuondosha kabisa changamoto ya kuwepo kwa hoja hiyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

32. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa Zanzibar ni mtumiaji mkubwa wa mboga za majani kwa ajili ya kuimarisha lishe za wananchi wake. Na kwa kuwa mahoteli ya kitalii yamekuwa watumiaji wakubwa wa mboga za majani kwa wateja wao. Na kwa kuwa mboga nyingi zinalimwa kwa kutumia mbolea na madawa yenye kemikali.

(a) Je, ni ipi tathmini ya utumiaji wa mboga za majani kwa mwaka 2024 hapa Zanzibar.

(b) Je, ni fedha za kiasi gani wakulima huingiza kwa kilimo cha mboga za majani hapa Zanzibar.

(c) Je, ni utaratibu gani Serikali imeutumia kuhakikisha mboga hizi zinakuwa salama kwa watumiaji.

269. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga skimu ya umwagiliaji katika shehia ya Mgagadu eneo la Kimbuni.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

206. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamatuni na Michezo:

(a) Ni utaratibu gani unaotumika kwa Wizara kufanya vikao na wadau wa sekta ya habari.

(b) Kwa kiasi gani vikao hivyo huibua matokeo chanya.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

130. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa skuli nyingi zimejengwa na nyengine kufanyiwa ukarabati. Na kwa kuwa skuli zipo ambazo hazina maeneo ya kujengwa skuli mpya na wanafunzi ni wengi.

Je, kuna mpango gani ulioandaliwa wa kulipatia ufumbuzi suala hilo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

72. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Miundombinu ya barabara ina umuhimu mkubwa na inahitaji uangalizi, wafanyakazi wa kuzitunza na kuziweka salama kwa mustakabali wa Taifa letu.

Ni utaratibu upi unaotumika kuzihudumia barabara zetu baada ya kukamilika kujengwa.

233. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) kwa kipindi cha mwezi wa Julai hadi Disemba, 2024 ilipanga kusajili meli 7 za ndani na kufanikisha kusajili meli 8 sawa na asilimia 114 ya makadirio, na kwa upande wa meli za kimataifa ilisajili meli 207 sawa na asilimia 172 ya makadirio.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea meli za nje kuwa ni nyingi kusajiliwa kuliko za ndani.

(b) Je, ni meli za nchi zipi zinazosajiliwa zaidi hapa Zanzibar.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

161. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Historia inatueleza kwamba takribani watumwa wasiopungua 50,000 walipitishwa Zanzibar kila mwaka na watumwa takribani 80,000 walifia njiani kabla ya kufika Soko Kuu la Watumwa, Kelele Square na hatimae Mkunazini.

(a) Je, jitihada za muendelezo wa kuzifufua njia walizopita watumwa hawa kutoka maeneo ya ndani Tanganyika hadi kufika katika Soko Kuu la Watumwa Zanzibar zina sura yoyote ya matumaini.

(b) Kwa nini Serikali haioni haja ya kuzifufua njia hizi wakati zitaongeza thamani na pato linalotokana na sekta hii ya utalii.

153. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni ipi historia halisi ya uwepo wa kanisa mashuhuri katika historia ya Zanzibar maarufu kwa jina la Kanisa la Waanglikana.

(b) Kwa nini watalii wengi duniani wanapendelea kulitembelea eneo hili.

(c) Kanisa hili lina mchango gani katika kuendeleza dhana ya uvumilivu wa kiimani na maridhiano ya kihistoria hapa Zanzibar.

**Zanzibar,**
**10 Juni, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**